

Bibilia ya watoto
Inawalettea

Mtu
Tajiri, Mtu
Masikini



Kimeandikwa na: Edward Hughes
Kimeorodheshwa na: Alastair Paterson; M.
Maillot; Lazarus
Imerekebishwa na: M. Maillot; Sarah S.
Kimetafsiriwa na: Bethel Children's Home,
Kisumu, Kenya and Emmanuel Menya
Kimedhibitishwa na: Bible for Children
www.M1914.org


BFC
PO Box 3
Winnipeg, MB R3C 2G1
Canada

©2020 Bible for Children, Inc.

License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii, lakini bila ya kuuza.




Yesu alijua kwamba viongozi wengi wa dini walipenda fedha kuliko kumpenda Mungu. Aliwaambia kuhusu kilichowapata watu wawili, na kwanini haina maana kuwa na utajiri bila Mungu. Utajiri hauwezi kununua uzima wa Mungu mbinguni.



Kulikuwa na mtu
fulani tajiri ambaye
alikuwa na nguo nzuri
sana zilizogharimu
fedha nyingi. Alivaa
kama mfalme.




Pia huyo tajiri alikula vizuri. Kila mlo ulikuwa kama sherehe kubwa. Alikuwa na fedha nyingi kiasi cha kuweza kununua chochote alichotaka kula asubuhi, mchana, jioni - au vitafunwa katikati ya mlo.



Katika lango la nyumba ya huyo tajiri alilala
ombaomba maskini, mgonjwa na anayekufa njaa.

Jina lake aliitwa Lazaro.



Maskini Lazaro alijaa vidonda. Yawezekana alikuwa na ugonjwa. Yawezekana alikuwa na michubuko kutoka kwa watu wasiomjali. Pengine alikuwa na vidonda kwasababu hakuwa na chakula kizuri kama maziwa, mboga za majani au nyama.



Lazaro alitamani
kupata chakula.
Alishukuru
kwa kupata
makombo
yaliyoanguka
chini ya meza
ya yule mtu
tajiri.




Mbwa wanaozurura
wakati mwingine
walimramba
ombaomba
masikini
asiyepata
msaada.


Walimnusa
na kuramba
majeraha yake.
Inaonyesha
hakuna mtu alijali
kwamba Lazaro
anakufa
njaa.



Asubuhi moja,
Lazaro hakuamka.
Ombaomba
masikini,
asiye na
rafiki aliondoka
katika maisha
haya. Lazaro
alikuwa amekufa.



Furaha ilianza kwa Lazao alipokufa tu. Yesu alisema kwamba malaika walimchukua awe pamoja na Ibrahimu. Lazaro alifarijiwa na Mungu.




Yule mtu tajiri naye pia akafa. Fedha zake zote hazikuweza kuokoa maisha yake. Kifo kilipokuja, hakuna mtu aliweza kukizuia.





Tajiri akazikwa. Labda yalikuwa ni mazishi makubwa. Labda watu walimsifu tajiri kwa kuwa mtu hodari na mwenye mafanikio. Lakini sifa zao hazikumsaidia. Tajiri alikuwa Kuzimu.




Kule Kuzimu, tajiri alilia, "Baba Ibrahimu, mtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake kwenye maji auburudishe ulimi wangu; kwavile ninateseka kwenye moto huu."



Ibrahimu akamkumbusha yule tajiri, "Katika maisha yako ulikuwa na kila kitu na Lazaro hakuwa na kitu. Sasa Lazaro anafarijiwa na wewe unaumizwa. Hakuna anayeweza kuvuka shimo kubwa lililoko kati yako na sisi."



Tajiri akasihi, "Mtume Lazaro akawaonye ndugu zangu watano. Sipendi wafike mahali hapa pa mateso."



Ibrahimu akamjibu, "Ndugu zako wana Neno la Mungu." Kama ndugu zako watano hawawezi kuiamini Biblia, hawataamini hata kama Lazaro atafufuka kutoka kwa wafu.



Yesu alipomaliza hadithi yake juu ya tajiri na Lazaro, labda viongozi wa dini walijiuliza maswali, "Napenda utajiri kuliko ninavyompenda Mungu?" Sasa walijua nini kitatokea kama hawatasikiliza Neno la Mungu.



Mtu Tajiri, Mtu Masikini

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Luka 16

“Kufafanusha maneno yako kwatia nuru.”

Zaburi 119:130





Mwisho

| 44

||||| 60



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na kumwomba msamaha kwa dhambi yako, Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani yako, na utaishi naye milele.

Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya kwa Mungu: Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na siku moja nitaenda kuwa nawe millele. Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila siku! Yohana 3:16

